Sudan Kusini

## Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 2

**Kiswahili kwa kidato cha Pili (2)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**
- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Kimefadhiliwa na:**


GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

Kiswahili 2

Kidato cha Pili



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia.**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
2

# Kiswahili

*Mwongozo wa Mwalimu*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION.
All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder. Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na: ya Elimu na Mafunzo.

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

FOREWORD

I am delighted to present to you this Teacher's Guide, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This Teacher's Guide shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum, school textbooks and Teachers' Guides for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum, the new textbooks and Teachers' Guides. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my role as the Undersecretary, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan

# YALIYOMO

SURA YA 1 : MAAMKUZI ........................................................................1
SURA YA 2 : UHIFADHI WA MAZINGIRA....................................................9
SURA YA 3 : UHIFADHI WA WANYAMAPORI..........................................17
SURA YA 4 : UNUNUZI NA UUZAJI WA BIDHAA ....................................25
SURA YA 5 : AFYA NA MAGONJWA ..........................................................37
SURA YA 6 : MILA, UTAMADUNI NA ITIKADI ....................................47

# SURA YA 1 :     MAAMKUZI

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**Maamkuzi**

**Funzo**:Maamkuzi

**Malengo maalum**:Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kuamkuana akizingatia msamiati ufaao katika muktadha wa shuleni
- Kuamkuana akizingatia nyakati za siku
- Kuzungumza kwa mfululizo huku akizingatia matamshi bora na sarufi mwafaka.
- Kujibu maswali ya salamu kwa usahihi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Mazungumzo ni mafunzo yaliyopewa kipa umbele katika mtalaa huu wa Kiswahili. Sababu ni kuwa, mara nyingi watu huwasiliana kwa njia ya kuzungumza. Na kabla ya kuanza kuzungumza au kusemezana ni lazima, kama ilivyo katika jamii yoyote ile kuamkuana kwanza. Kuamkuana huleta watu pamoja na kuteka makini ya msemewa. Kwa hivyo, ni maamkuzi ni lazima kama sharia. Kisha mazungumzo hufuata. Ni vyema mwanafunzi kujua mazungumzo huathiriwa na mambo mengi kama vile dini, umri, rika, mazingira, mada, na kadhalika. Ni vyema mwanafunzi kufahamu na kujizoesha sajili mbalimbali ili aweze kukuza na kutumia msamiati na kaida zifaazo za mazungumzo. Wape wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi ya kuongea darasani huku ukiwaelekeza kuhusu msamiati, matamshi na kanuni nyingine muhimu kulingana na sajili inayohusika. Vilevile ingefaa uwahimize kutumia Kiswahili nje ya darasa huku wakizingatia msamiati ufaao kulingana na sajili. Pia waelekeze kusoma tamthilia, riwaya na hata magazeti ya Kiswahili na baadaye uwaongoze kujadili maamkuzi yaliyomo. Mwalimu, usisahau kuwapeleka sehemu mbalimbali za mahusiano ili kusikia vile wanavyoamkuana na watu katika jamii. Himiza adabu na heshima katika shughuli zote.(Maelekezo haya utayatumia mara kwa mara katika sehemu ya kusikiliza na kuzungumza.)

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali kadha kuhusu maamkuzi katika muktadha wa darasani.
- Waagize wawili wao kuja mbele ya darasa na kuamkuana.Wabadilishane kulingana na umri, jinsia, dini na miktadha kama rasmi na isiyo rasmi. Wape mwongozo kuhusu msamiati ufaao katika muktadha mahususi.
- Waongoze kusoma maaamkuzi yaliyomo kati kitabu kulingana na wakati. Kisha waelekeze kuyatumia maamkuzi hayo. Wachague wawili wawili kusoma huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji bora. Hakikisha kuwa wengi wao iwezekanavyo wamepata nafasi ya kusoma na kuigiza.
- Waite wawili wawili kuja mbele ya darasa wakiwa na vitabu vya kusoma na wajaribu kuigiza mazungumzo hayo huku ukiwapa maelekezo.
- Wapatie muda wa kutaja msamiati na pia mjadili maana za msamiati mwingine wasiouelewa. (Utaratibu huu utautumia mara kwa mara katika sehemu za: kusikiliza na kuzungumza ili kujenga stadi za kusikiliza, kuzungumza na msamiati.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo na kuwashauri vilivyo. Tathmini mazungumzo watakayoyaandika na kuhakikisha kuwa yanafuata kanuni za mazungumzo.

**Majibu**

1. Wanafunzi wataje salamu na mwitikio wake katika mazungumzo kama ifuatavyo:
    a) Sabakheri? - Alkheri!
    b) Umeamkaje leo? - Nimeamka salama salimini!
    c) Waambaje? - Naamba salama!
2. Kulingana na kifungu,Ali aliporudi nyumbani jioni Zaina alikuwa ameenda kumtembelea nyanya kumpa pole kwa vile hakujihisi vizuri.
3. Nyumba ya nyanya iko karibu na barabara na ina paa ya rangi nyekundu, Karibu kuna mti mkubwa ajabu.
4. Maana ya nyakati:

a) asubuhi - wakati jua linaanza kuchomoza
b) magharibi - wakati jua linaenda kutua
c) alasiri - wakati wa saa nane hadi saa tisa.
d) usiku - wakati jua limetua na giza limeingia

e) mchana - wakati ambao jua limechomoza hadi litue/ kinyume cha usiku

## KUSOMA

### Shairi

**Funzo**: Ufahamu – Shairi

**Malengo maalum**: Baada ya funzo mwanafunzi aweze:

- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kupanua msamiati wa kuamkuana kwake.
- Kusoma kifungu na kujibu maswali yanayofuatia.

**Vifaa**

Makala mbalimbali kutoka magazetini na majaridani kuhusu maamkuzi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kama tulivyosema hapo awali, siku njema huonekana asubuhi. Maamkuzi ni kipengele muhimu sana katika jamii. Kujua aina mbalimbali za maamkuzi na wakati wake ni bora Zaidi. Kwa hivyo, ni jukumu lako mwalimu kutafuta mbinu mwafaka kumwezesha mwanafunzi kujua maamkuzi ya aina mbalimbalimbali. Vilevile, maamkuzi huambatana na matamshi bora. Hisia katika mazungumzo na maamkuzi ziweze kudhihirika kwa mwanafunzi kutamka maamkuzi ipasavyo. Kwa hivyo, kuwa mwanga wa kuwaelekeza kutamka na kuthihirisha hisia mwafaka. Kwa mfano: kuna tofauti ya hisia baina ya 'makiwa' na 'umeamkaje'. Kuwa kielelezo na mwanga wa matumaini.

**Utaratibu**

- Waelekeze kuhusu somo kwa kuwauliza maswali ya dodoso kama vile:
  - a) Taja salamu za asubuhi.
  - b) Je, kuna haja ya kudhihirisha hisia wakati wa maamkuzi?
  - c) Mtu anapokuongelesha bila kukuamkua unahisi vipi?
  - d) Je, maamkuzi ni muhimu katika jamii?

**Tathmini**

Waongoze kujibu maswali yaliyomo kisha uyasahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1.Wanafunzi wajibu salamu kulingana na shairi. Mwalimu hakiki majibu ya wanafunzi.

i. Habari za asubuhi? - **Nzuri/Njema!**
ii. Umeamkaje? - **Nimeamkasalama/Vyema!**
iii. Habari za mchana? - **Nzuri/Njema/Salama!**
iv. Umeshindaje? - **Nimeshinda salama/Vyema!**
v. Alamsiki! - **Binuru!**

2. Wanafunzi waweze kutambua salamu na mwitikio waliopewa.

i. **Salamu za mchana**

Habari za mchana? - **Habari za mchana njema!**
Umeshindaje? - **Nimeshinda salama salimini.**

ii. Salamu za usiku

Alamski! - **Binuru!**
Usingizi wa pono! - **Nawe pia!**

3. Taja salamu nne unazoweza kummwamkua mtu wakati wowote.

i. Hujambo? - **Sijambo!**
ii. Hamjambo? - **Hatujambo!**
iii. Salaam aleikum? - **Aleikum salaam!**

## SARUFI

## Nyakati

**Funzo**: Nyakati

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua kitenzi katika sentensi.
- Kutambua wakati uliotumika katika sentensi.
- Kutambua kitenzi kilicho na kiambishi cha wakati.
- Kutumia wakati uliopita na ujao kwa usahihi.
- Kujibu maswali mbalimbali kuhusiana na nyakati.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwakumbusha wanafunzi kuhusu vitendo walivyofanya siku iliyopita ukitumia maswali ya dodoso kama vile:
  a) Juma, jana ulifanya nini?
  b) Kitenzi ni kipi katika sentensi ambayo (Juma) umesema?
  c) Kiambishi cha wakatiki ni kipi katika sentensi hiyo?
  d) Wakati nini?
  e) Mnajua nyakati ngapi? (na kadhalika).
- Waelekeze kupitia maelezo yaliyomo kitabuni. Waambie wasome sentensi kuhusu nyakati huku ukiwapa mifano na ufafanuzi zaidi. Pia waongoze kutoa mifano ya ziada kuhusu nyakati katika sentensi.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kisha usahihishe na kuwashauri ipasavyo.

**MAJIBU**

**1.Wanafunzi watambue na kupigia mstari viambishi.**

Mwalimu hakiki majibu.

i. Nini <u>kitamleta</u> kwangu kesho?
ii. Khadija na Ali <u>wataenda</u> sokoni.
iii. Siku hiyo <u>nitalima</u> shamba letu.
iv. UKIMWI <u>utawaacha</u> watoto wengi mayatima.
v. <u>Atamfikisha</u> karibu na kwao.

**2. Majibu kutoka kwenye mabano ni:**

i. Siku baada ya leo ni **kesho**.
ii. Wakati wa saa sita mchana huitwa **adhuhuri**.
iii. Mapema wakati wa kuamka huitwa a**subuhi**.
iv. Unapoambiwa alamski unajibu **binuru**.
v. M**agharibi** ni wakati wa jua kutua.
vi. Unapofika njia panda unachagua kushoto au **kulia**.
vii. S**hikamoo**ni salamu ya wadogo kwa wakubwa.

viii. Wakati baina ya kuchomoza na kutua kwa jua huitwa **mchana**.
ix. **Usiku** ni wakati wa kulala.
x. Salamu ya sabalkheri hujibiwaje? A**lheri!**

**3. Kujaza kifungu kwa neno mwafaka na wakati.**
Mama alipoamka asubuhi na mapema,alitusalimia **sabakheri**nasi tukamjibu alheri.Kakangu alimwamukua shikamoo naye mama akamjibu **marahaba**.Ilikuwa siku yangu ya kupeleka mifugo malishoni mpaka **alasari**yaani saa nane mpaka saa kumi kamili.Nilimuaga mama,"Kwaheri" huku akijibu **kwaheri ya kuonana**.Baadaye wakati wa**magharibi,**jua, likitua nilirudisha mifugo nyumbani.

**4. Kugeuza maneno yaliyokolezwa wino katika wakati ujao-ta-**
Mtihani wa somo la Kiswahili **utafanywa** kesho kutwa. Wanafunzi wote **watatarajiwa** kubeba vifaa vya kuandikia. Kila mwanafunzi **atakuw**a na nakala moja ya maswali. Mwalimu **atatembea** darasani kuhakikisha nidhamu wakati wa mtihani. Wanafunzi **wanafanya** mtihani kwa muda wa saa mbili. Mwalimu **atakusanya** mitihani na **atawapatia** walimu wasahihishe.

5. Kutaja wakati wa kuamkuana salamu.

| | | |
|---|---|---|
| i. | Sabakheri? | **asubuhi** |
| ii. | Binuru! | **usiku** |
| iii. | Hujambo? | **wakati wowote** |
| iv. | Kwaheri! | **watu wanaoagana** |
| v. | Safari njema! | **mtu anapoenda safari** |
| vi. | Makiwa! | **mtu akiwa amefiwa** |
| vii. | Pole kwa ugonjwa | **mtu anapougua** |
| viii. | Tafadhali! | **unapoomba hisani kwa mtu** |
| ix. | Lala salama! | **wakati wa kwenda kulala** |
| x. | Nisamehe! | **unapomkosea mtu** |

**6. Kujaza pengo kwa neno la adabu na heshima.**
**1.**Ikiwa umemkosea mtu na unataka akusamehe utamwambia n**isamehe**au **naomba msamaha**.
1.Mwenzako amepata ajali utamwambia **pole**.

2.**Asante**ni tamko la kurudisha shukrani.
3.**Sumile!** nipishe nataka kupita.

## KUANDIKA

**Funzo** : Insha ya mazungumzo.

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya insha ya mazungumzo.
- Kutaja sifa za insha ya mazungumzo.
- Kuandika insha nzuri ya mazungumzo.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uandishi wa insha kwa jumla, kwa mfano:
  a) Insha ni nini?
  b) Ni mambo gani yanayofaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
  c) Insha ya mazungumzo ina sifa zipi?
- Waelekeze kusoma kimya mazungumzo katika magazeti na majarida. Kisha, chagua wawili wa kusoma nafasi za wahusika huku mwingine mmoja akisoma maelezo mabanoni. Wasome kwa sauti huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji ufaao hasa wa matamshi, sarufi, kiimbo na kadhalika.

**Tathmini**

- Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri zaidi.
- Hakikisha kuwa wanafunzi wameandika insha hii ya mazungumzo. Isahihishe na kuwashauri vilivyo.
- Hakikisha:

1.Wanafunzi wameandike kisa kwa mtindo wa mazungumzo.
2.Lugha inayoambatana na kupanga miadi inafuatwa.
3. Mazungumzo yanazingatia msamiati wa salamu baina ya:
   i. Mtoto na mzazi
   ii. Mjukuu na babu yake
   iii. Vijana wawili

4. Lugha inayotumika kwa kila mazungumzo iafikiane na kiwango cha wahusika waliotajwa. Kwa mfano, lugha ya mtoto na mzazi iwe tofauti na ya mjukuu na babu yake au ya vijana. Hili jambo la muhimu kwa sababu, mazungumzo na mada hutegemea uhusiano na umri baina ya wazungumzaji.

**Zoezi la ziada**

Wape nafasi ya kwenda kusoma mazungumzo hayo tena kwa nia ya kuyaigiza darasani. Baadaye waongoze kuigiza kisha uzue mazungumzo kutokana na uigizaji huu yatakayowashirikisha wanafunzi wote.

# SURA YA 2 : UHIFADHI WA MAZINGIRA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Shairi

**Funzo**: Kukariri shairi

**Malengo maalum**: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- kufotautisha kati ya shairi huru na lile la arudhi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na sifa na tofauti baina ya mashairi ya arudhi na yale huru – mbona hili liitwe la arudhi' na lile huru'? Pia elewa kuwa wanafunzi wengi huamini kuwa mashairi ni sanaa ngumu inayotaka 'malenga' pekee. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Waeleze na kuwaonyesha arudhi: mizani, vina, muwala na utoshelezi kwa jumla. Waeleze pia kuhusu matumizi ya uhuru wa mwandishi huku ukiwaonyesha mpaka wa uhuru huo ili wasiboronge lugha kiholela wakidhani wanatumia 'uhuru'. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa umewatungia shairi fupi la kuwatolea mfano. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
  - a) Taja kwa jumla, sifa za mashairi.
  - b) Ni vipengele gani muhimu unavyopaswa kuzingatia katika kukariri shairi?
  - c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri.

Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu mazingira na utunzi wake.

**Tathmini**

- Waelekeze wanafunzi katika kujibu maswali waliyoagizwa. Unaposahihisha ona kuwa silabi na maneno yameandikwa kuzingatia sarufi wala si kuboronga jinsi ilivyo katika shairi.
- Mwanafunzi atumie lugha ya kinathari kujibu maswali huku akizingatia ujumbe.

**Majibu**

1. Kupunguza maafa,chanzo cha mvua, kuongezeka kwa mazao na kufaidika kwa kizazi kijacho.
2. Maneno, " Shiriki pasi kusita, maji yasije gharimu"katika ubeti wa 3 yana maanisha kila mmoja ajitokeze kulinda na kuhifadhi chemchemi za maji ili mambo yasiharibike yakiharibika maisha yatakuwa ya gharama ya juu.
3. Madhara ni magonjwa, kusononeka, kufa kwa wanyama.

## KUSOMA

### UHARIBIFU WA MAZINGIRA

**Funzo**: Ufahamu – Uharibifu wa mazingira

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kutaja na kufafanua mbinu za utanzaji na uharibifu wa mazingira.
- Kujibu maswali yanayotokana na kifungu cha ufahamu kwa usahihi.

**Vifaa**

Picha, michoro na mabango kuhusu mazingira; kwa mfano, wakikata miti, wakichoma makaa, watu wakilima kwenye milima, viwanda vikimwaga kemikali na majitaka mitoni, magari makuukuu yakitifua moshi na mafuta yakimwagika baharini.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Katika siku za hivi karibuni, suala la utunzaji mazingira limepewa uzito sana katika nchi yetu na ulimwengu kwa jumla. Sababu ni kuwa, mazingira yakiharibiwa tutakuwa katika balaa kubwa.Miti imekuwa ikikatwa ovyoovyo, majitaka kutoka viwandani yanamwagwa kivoloya mitoni na mabwawani. Mazingira yamekuwa si mazingira tena. Misitu inafyekwa ili kujenga miji. Mazingira haya ni yangu na wewe. Kila mmoja awajibike na kutunza mazingira. Tusikate miti ovyo, tusilime karibu na chemchemi za maji, tusichome makaa na kuzidisha moshi kuharibu ozoni. Katika mtalaa wa Kiswahili, hili ni mojawapo ya masuala yalilotiliwa mkazo. Lengo ni kuhakikisha kuwa suala la mazingira, walimu na wanafunzi wanalipa kipa umbele. Hakikisha kuwa umewapa nafasi ya kuongea bila upingamizi wowote kuhusu mazingira hasa baada ya kusoma kifungu hiki. Unaweza kuwapa nafasi ya kushiriki katika midahalo kati yao na vidato vingine hapo shuleni au kati yao na shule jirani kuhusu masuala haya ya mazingira ili wazidi kuhamasika zaidi na kuelewa mengi kuhusu jambo hili muhimu katika maisha yao.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uharibifu wa mazingira kama vile:

  a) Je, kukata miti kuna athari gani?
  b) Je, ni vizuri viwanda kuwachilia moshi kupaa angani?
  c) Je, ni vizuri kuoga mtoni?
  d) Je, ni magari yanayopiga muziki wa juu yakubaliwe barabarani?
  e) Taja mambo yoyote yanayoharibu mazingira.
- Soma aya ya kwanza kwa sauti huku ukizingatia usomaji mwafaka ili uwe kielelezo kwa wanafunzi wako.
- Waagize kusoma kwa sauti huku ukiwakosoa na kuwaelekeza kuhusu usomaji ufaao. Kila mwanafunzi anaweza kusoma aya moja. Hakikisha kuwa wengi wao wamepata nafasi ya kusoma hasa wale walio na shida za usomaji. Kwa mfano, iwapo kuna mwanafunzi ambaye hugugumiza anaposoma, mpe nafasi zaidi ya kushiriki katika usomaji na uhakikishe kuwa hachekwi au kufanyiwa mzaha na yeyote darasani eti kwa vile ana shida ya kusoma. Ni

bora uwafunze wanafunzi wako umuhimu wa kuheshimiana na kuthaminiana.

- Baada ya kusoma waongoze kujadili msamiati wasioufahamu pamoja na masuala mazito yaliyojitokeza. Unaweza kuwaelekeza kutunga sentensi wakitumia baadhi ya msamiati ili kuthibitisha maana yake.

**Tathmini**

- Waulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa kwa mdomo wala si kwa kuandika.
- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Vijembe na mikebe ya kila aina, sindano zilizotumiwa, misumari na vifaa vingine vya kudungia.
2. Viongozi na wananchi wapenda Amani
3. Viwanda vingi **hufusha moshi** ambayo haichukizi tu bali huweza kusababisha magonjwa ya saratani ya mapafu na pumu.
4. Kwa kutupa karatasi ovyo, kuchonga kalamu zao za mate na kuacha taka kokote darasani,kukata nyasi na matawi ya miti na kuyaacha yatapakae kote badala ya kuyachoma.
5. Kupata nyama na wengine wapate vipusa vya vifaru
6. Huzidisha tatizo la mmomonyoko wa udongo
7. Sehemu hizo zimegeuzwa kuwa misala na mabafu ya kuoshea nguo.
8. Kipindupindu,homa ya matumbo,pepopunda, saratani ya mapafu na pumu.
9. Kwa sababu ya kutojenga wa kujenga misala.
10. Kuenea kwa jangwa.
11. Watalii wakikoma kuja kututembelea pesa za kigeni zitaendelea kuwa haba na uchumi wetu utadidimia.
12. Vyombo vya baharini, viwanda na magari makuukuu.
13. Viumbe wa baharini kama vile samaki kwa moshi wa vyombo vya baharini na wanyama wanaoishi ndani ya udongo kupitia kemikali nyingi zinazonyunyuziwa mashamba
14. Ndiyo, huharibu viwambo vya masikio kwa sababu ya kelele
15. 
    i. umekithiri -umezidi

ii. mabiwi -mapipa yataka (taka nyingi)
iii. hufusha moshi -hutoa moshi
iv. viwambo vya masikio -sehemu ya sikioinayopokea sauti
v. tunu -zawadi/tuzo/kitu cha thamani kubwa

**Kazi ya ziada**

Wape wanafunzi kazi hii waifanyie utafiti. Watazoea na kujua umuhimu wa kutunza na madhara ya kuharibu mazingira.

**Jadili na mwenzako madhara yanayosababishwa na viwanda.**

## SARUFI

**Matumizi ya -nge- na -ngali-**

**Funzo** : Matumizi ya -nge- na -ngali-

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya -nge- na -ngali-.
- Kutumia -nge- na -ngali- kwa usahihi.
- Kukanusha matumizi ya -nge- na -ngali- kwa usahihi.
- Kujibu maswali mbalimbali kuhusiana na -nge- na -ngali-.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwakumbusha wanafunzi kuhusu ngeli na upatanisho wa kisarufi ukitumia maswali ya dodoso kama vile:
  a) Nomino katika ngeli ya A-WA ni zipi?
  b) Ukitumia nomino katika ngeli ya A-WA kiambishi kipi kitawekwa sehemu ya awali ya -nge- na -ngali-?
  c) Ni nani amewahi kusikia matumizi ya -nge- na -ngali-?
  d) Je, tunaweza kukanusha -nge- na -ngali-?
- Waelekeze kupitia maelezo yaliyomo kitabuni. Waambie wasome sentensi kuhusu -nge- na -ngali- huku ukiwapa mifano na ufafanuzi zaidi. Pia waongoze kutoa mifano ya ziada kuhusu hali za masharti haya.
- Waelekeze wanafunzi wa kutunga sentensi wakitumia hali za masharti haya. Waelekeze na kuwashauri ipasavyo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya mazoezi yaliyomo kisha usahihishe na kuwashauri.

**Majibu**

**1.Maana ya sentensi kwa ufasaha:**

i. Hawajala kwa sababu hawakupika.
ii. Walikopa ndipo wakalipa.
iii. Hawakumlipa kwa sababu hawakuwa na pesa.
iv. Alikamatwa kwa sababu aliiba.
v. Hakupita mtihani kwa sababu hakusoma.

**2. Kukanusha**

i. Asingekuja asingemwokoa.
ii. Wasingegombana wasingepigana.
iii. Tusingalisafiri tusingalifika.
iv. Msingaliimba jana msingalishinda.
v. Asingemchukua mtoto huyoasingemlea.
vi. Nisingalisikiliza nisingalipona.
vii. Asingerudi mapema asingenisaidia.
viii. Wasingalishiba wasingalilima.
ix. Tusingemwonya mapema asingebadilika.
x. Nisingekata tamaa mapema nisingeshindwa.

**3. Kuandika katika hali yakinifu.**

i. Ningemkimbilia ningeanguka.
ii. Tungalikuwa wachoyo tungalikufa njaa.
iii. Mtoto angalikufa wazazi wangalihuzunika.
iv. Kilio kingalitanda arusi ingalisimamishwa.
v. Mnyama angepatikana kafara ingefanyika.
vi. Tungalifika mapema tungalimpata.
vii. Mngemtembelea juziangelemewa sana.
viii. Ningalilima sana ningalipata mavuno.
ix. Gari lingemgonga askari wangekuja.
x. Barua ingeandikwa mapema mwanafunzi angeenda.

**4.**Kutunga sentensi kwa -nge- au -ngali- kwa kutumia maneno yaliyopeanwa. Mwanafunzi azingatie sarufi katika utunzi wa sentensi.

**5.** Wanafunzi watunge sentensi tano kwa kutumia ukanusho wa **ngali.**

Mfano: Kama angalisoma hangalifaulu.

Mwalimu, hakikisha wanafunzi wamezingatia swali na sarufi.

**6**. Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia msamiati wa mazingira.Mwalimu hakikisha sentensi ni sahihi na zina ujumbe.

## KUANDIKA

**Funzo**: Insha ya maelezo.

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya insha ya mazungumzo.
- Kutaja sifa za insha ya mazungumzo.
- Kuandika insha nzuri ya mazungumzo.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uandishi wa insha kwa jumla, kwa mfano:
  a) Insha ni nini?
  b) Ni mambo gani yanayofaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
  c) Insha ya maelezo ina sifa zipi?
- Waelekeze kusoma kimya vifungu katika vitabu, magazeti na majarida kuhusu mazingira.
- Chagua wanafunzi ili waeleze mambo yanayosababisha uharibifu wa mazingira. Waelekeze jinsi ya kutumia lugha ya kushawishi na kutahadharisha dhidi ya utunzi na uharibifu wa mazingira. Wanapozungumza, tilia mkazo kiimbo na shadda ili lugha ivutie, ishawishi na kutahadharisha kutegemea na jambo analozungumzia.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri zaidi. Hakikisha kuwa wanafunzi wanaandika insha hizi kwa wakati tofautitofauti ili kukuza na kuwaelimisha umuhimu wa kutunza mazingira.

Hakikisha unasahihisha insha hizo ukiwaelekeza na kuwashauri vilivyo.
Hakikisha:

1.Wanafunzi wanaandika insha kwa mtiririko mwafaka.
Wanatoa hoja kwa upande wa manufaa ya kuhifadhi mazingira. Kwa mfano, kuepuka magonjwa,miti inaleta mvua,kuepuka ajali,kwa mfano, kukatwa na vioo vilivyotupwa ovyoovyo. Huvutia watalii na kadhalika.
2.Wanafunzi waorodheshe mambo yanayosababisha uharibifu wa mazingira. Kwa mfano, ukataji miti,kuua wanyama pori,kutupa taka ovyoovyo,kuchafua mito na kadhalika.
3.Wanafunzi waandike njia mbalimbali za kuzuia uharibifu wa mazingira. Kwa mfano kupanda miti na kutokata miti,kutochafua mito,kuchimba majaa ya kuweka taka na kadhalika.

# SURA YA 3 : UHIFADHI WA WANYAMAPORI

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Shairi

**Funzo**: Kukariri shairi

**Malengo maalum**: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusikiliza kwa makini
- Kukuza msamiati wake.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na kusikiliza kwa makini na kutamka maneno kwa usahihi. Buni mbinu mbalimbali za kukuza matamshi hata ikiwa ni nyimbo, mijadala, mazungumzo na hotuba. Kukuza kipawa cha kuzungumza hadharani na kutamka kwa usahihi maneno na silabi ni jambo muhimu. Vilevile, kutilia mkazo, shadda, kiimbo na toni. Kwa hivyo, mashairi na nyimbo kama sanaa vitawawezesha kuchangamkia Kiswahili na hiyo itakuwa hatua nzuri katika kufunza na kuwahamasisha na lugha hii. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa unakariri na kutamka maneno kwa ufasaha mno. Zingatia shadda na kiimbo. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
    a) Nani amewahi kumsikia manju akiimba/akikariri shairi?
    b) Ni vipengele gani muhimu unavyopaswa kuzingatia katika kukariri shairi?

c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?

-  Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu wanyamapori na jinsi ya kuwatunza.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi katika kujibu maswali waliyoagizwa. Unaposahihisha ona kuwa silabi na maneno yameandikwa kuzingatia sarufi wala si kuboronga jinsi ilivyo katika shairi. Mwanafunzi atumie lugha ya kinathari kujibu maswali huku akizingatia ujumbe.

**Majibu**

1. Kuwaona wanyama pori.
2. Miji imekua,mapori yamepanuka,hela za kigeni zinapatikana.
3. Majangili/wawindaji.
4. Kwa sababu watu wanawaua kwa ajili ya pembe,kwato, wanasumbuliwa, wanauliwa kila uchao na mapori yaoyanavamiwa/yanaangamizwa.
   (Hakiki majibu ya wanafunzi.)

## KUSOMA

### WANYAMAPORI

**Funzo**: Kusoma kwa sauti - Wanyamapori

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusoma kifungu kwa sauti na ukakamavu akizingatia matamshi bora, shadda na kiimbo na alama za kuakifisha.
- Kujibu maswali kwa usahihi.
- Kueleza manufaa ya kutunza wanyamapori na mbinu za kukabiliana na majangili.

**Vifaa**

Magazeti, majarida na vitabu mbalimbali ya Kiswahili

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kusoma ni stadi muhimu sana. Binadamu anahitajika kusoma mambo mbalimbali katika maisha yake ya kila siku. Husoma vitabu, magazeti, majarida, barua na maandishi mengine mengi. Kwa sababu hii, ni muhimu sana mwanafunzi kuzidi kuelekezwa kuhusu stadi hii ya kusoma ili aweze kuimarika ipasavyo.

Njia moja ya kufanya hivyo ni kuwapa nafasi ya kusoma magazeti na majarida ya Kiswahili katika maktaba ya shule na kuwahimiza kuyasoma kwingineko hasa nyumbani na katika maktaba za umma. Kwa hivyo, ni wajibu wako kuhakikisha kuwa magazeti ya Kiswahili yanapatikana hapo shuleni. Shule nyingi hazijishughulishi sana kununua magazeti ya Kiswahili bali hununua tu yale yaKiingereza. Hakikisha kuwa jambo hili halifanyiki ikiwa unataka kuwafaa wanafunzi wako kumudu mafunzo kama haya ya barua kwa mhariri na pia kuwaonyesha umuhimu wa Kiswahili katika mawasiliano.

Licha ya kusoma, ni vyema wanafunzi kuangaziwa kuhusu umuhimu wa kutilia maanani na kutafakari kuhusu hoja mbalimbali zinazojitokeza katika ufahamu. Mambo hayo huwa ya manufaa mbalimbali kwa umma. Pia unaweza kuwahimiza kuandika makala za aina hii na hata kuyatundika darasani. Vilevile unaweza kuwahimiza kutafuta makala kuhusu uhifadhi wa wanyamapori.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na barua kwa mhariri kama vile:
  a) Wanaona nini katika picha?
  b) Je, kuna picha inayodhihirisha kuhatarisha maisha ya wanyamapori
  c) Wanyamapori wana umuhimu gani katika jamii?
  d) Wanyama hao hutunzwa na nani?
  e) Barua hizi huandikwa na nani?
  f) Wanyama hao wako katika hatari gani?
  g) Je, tutawatunzaje wanyama hao? na kadhalika.
- Huku ukitumia magazeti mbalimbali kufafanulia, waelekeze kusoma maelezo yaliyomo kitabuni na kuwatolea ufafanuzi zaidi.
- Waelekeze kusoma na kuchambua baadhi ya makala ya utunzi wa

wanyamapori kabla ya kusoma kifungu katika kitabu chao.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kitabuni kisha ulisahihishe na kuwashauri zaidi.

**Majibu**

1. Tembo na kifaru, kwa sababu ya pembe zao, meno na kwato
2. 
   i. Ni pato kwa taifa,
   ii. watalii kuzuru nchi
   iii. ajira kwa watu
3. Ni kwa manufaa yao wenyewe.
4. 
   i. Kuhakikisha ulinzi shirikishi baina ya wananchi na serikali,
   ii. serikali kuweka wazi mapato yatokanayo na sekta ya utalii kwa umma,
   iii. sheria zilizotungwa dhidi ya majangili ziwe wazi pasipo kupendelea mtu,
   iv. kuhakikisha hifadhi za wanyama pori zinakuwa salama.
5. Kushuka kwa pato linalopatikana kutokana na wanyama hao.

## SARUFI

### Wakati uliopo na Wakati ujao

**Funzo:**Nyakati: wakati uliopo na ujao

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua viambishi vya wakati katika vitenzi
- Kutambua wakati uliotumika katika sentensi
- Kutumia wakati mwafaka katika sentensi.

**Vifaa**

Magazeti, mabango, chati na michoro

**Utaratibu**

- Anza kwa kufanya kitendo nao wakisema unafanya nini?
- Andika sentensi hizo ubaoni.
- Waulize jana walifanya nini?
- Andika sentensi hizo ubaoni.
- Waulize kesho watafanya nini?
- Andika sentensi hizo ubaoni.
- Waulize maswali ya dodoso kuhusu tofauti katika sentensi hizo kiwakati.
- Waongoze kupitia sentensi hizo wakitambua viambishi vya wakati ukiwaelekeza ni wakati gani.
- Waongoze kusoma sentensi katika kitabu cha mwanafunzi huku wakitoa mifano zaidi.
- Ukitumia vitabu vya riwaya, tamthilia, hadithi fupi au magazeti, pitieni pamoja huku mkibainisha matumizi ya nyakati katika sentensi.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mawaidha zaidi.

**Majibu**

**a) Wati uliopo na wakati ujao**

| **Kitenzi** | **Wakati uliopo** | **Wakati ujao** |
|---|---|---|
| 1. lima | A**na**lima. | A**ta**lima. |
| 2. shuka | A**na**shuka. | A**ta**shuka. |
| 3. lia | A**na**lia. | A**ta**lia. |
| 4. kimbia | A**na**kimbia. | A**ta**kimbia. |
| 5. omba | A**na**omba. | A**ta**omba. |
| 6. fariji | A**na**fariji. | A**ta**fariji. |
| 7. soma | A**na**soma. | A**ta**soma. |
| 8. ngoja | A**na**ngoja. | A**ta**ngoja. |
| 9. osha | A**na**osha. | A**ta**osha. |

**b) Kuandika sentensi katika wakati uliopo**

1. Ndugu yangu anatembelea bunga la wanyama.
2. Ndovu anaharibu mimea shambani.
3. Ninamwona fisi akila.

4. Mtoto wa ndege anaitwa kinda.
5. Baba anampiga picha swara.
6. Nyani wanaishi mitini.
7. Wanyama pori wanahitaji kulindwa.
8. Msasi ni mtu anayewaua wanyama pori.
9. Anakamatwa kwa kumuua ndovu yule.
10. Misitu inatumika kama makaazi ya wanyama pori.

**c) Kutambua nyakati katika sentensi?**

1. Watamtembelea lini? (**wakati ujao)**
2. Nani anataka kumwona tumbili? (**wakati uliopo)**
3. Wanamazingira watachunga miti hiyo. (**wakati ujao)**
4. Nyoka watapatikana msituni. **(wakati ujao)**
5. Mwezi ujao tutapanda miti. **(wakati ujao)**
6. Simba anaogopwa na binadamu. (**wakati uliopo)**
7. Fisi anakula nyama iliyooza. (**wakati uliopo)**
8. Uhifadhi wa wanyama unafanyika. (**wakati uliopo)**
9. Ngozi ya chui inatengeneza bidhaa kadhaa. (**wakati uliopo)**
10. Pembe za ndovu zitapatikana mwakani. (**wakati ujao)**

**d) Kupigia mstari maneno yaliyotumia wakati uliopo na wakati ujao katika kifungu hiki**

Wanyama pori wanapaswakulindwa kwa kila njia.Wasasi watakaopatikana wakiwawinda wanyama hawa watakamatwa.Nchini mwetu tunahamasishwa juu ya umuhimu wa wanyama hawa wa porini.Binadamu atanufaika kwa kiwango kikubwa kwa kutowaua wanyama hawa.Ninapochunguza faida za kuwahifadhi,ni nyingi mno kuliko hasara.Tunapotembelea**m**bunga za wanyama,tunafurahiakuwaona.Kizazi kijacho kitanufaikakwa kuwaona wanyama hawa wa pori.

**e) Kuandika wakati uliotumika katika kila sentensi**

1. Mwindaji anaachiliwa lakini atakamatwa.(wakati uliopo, wakati ujao)

2.Tumbili anambeba mtotowe na baadaye atapotea.
(wakati uliopo, wakati ujao)

3.Serikali itajenga ua utakaozuia maangamizi ya anyama pori.
(wakati ujao,wakati ujao)
4. Tumbili watakaovamia shamba lake wanajificha mtini.
(wakati ujao,wakati uliopo)
5. Mkulima atawawinga ndovu wanaomharibia mazao.
(wakati ujao,wakati uliopo)

**f) Kutunga sentensi sabakwa kutumia wakati ujao.**

**(Mwalimu, hakiki sarufi katika sentensi na hakikisha ziko katika wakati ujao)**

**g) Eleza maana ya msamiati wa wanyama pori ufuatao**

i. majangili – wawindaji haramu wa wanyamapori
ii. wanyamapori – wanyama wanaoishi mwituni/kinyume na wanyama wa nyumbani
iii. shirika la huduma kwa wanyama – Idara ya serikali inayohifadhi wanyamapori na misitu
iv. zuu – sehemu ya kuhifadhi wanyamapori
v. mbuga za wanyama – maeneo ya misitu wanakohifadhiwa wanyamapori

## KUANDIKA

**Funzo**: Insha za maelezo na mjadala

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

-  Kueleza maana ya insha ya maelezo na mjadala.
-  Kutaja sifa za insha ya maelezo na mjadala.
-  Kuandika insha ya maelezo na mjadala.

### Vifaa

Kanda za kunasia sauti zenye maelezo na mijadala, makala kutoka katika magazeti, majarida na vitabu.

### Utaratibu

-  Wakumbushe sifa za insha ya maelezo na mjadala kwa maswali ya dodoso kama vile:

a) Maelezo/mjadala ni nini?
b) Hutolewa kwa madhumuni gani?
c) Hutolewa na nani?
d) Huwa na sifa zipi?
e) Huwa na urefu gani? na kadhalika.

- Ikiwezekana wachezee kanda zenye maelezo/mjadala za watu mashuhuri waliojulikana kwa kueleza jambo au kujadili jambo kisha mzichambue.
- Waongoze kusoma maelezo na mijadala katika vitabu huku ukiwafafanulia zaidi. Washirikishe kwa kuwauliza maswali mbalimbali katika kila hatua.

**Tathmini**

- Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauriipasavyo.
- Wanafunzi wazingatie mada zifuatazo:

1.Andika insha juu ya umuhimu wa kuhifadhi wanyamapori.
2.Andika faida zinazopatikana kutoka na wanyamapori.
3.Mbuga za wanyamapori zina manufaa kwa nchi.Jadili.

# SURA YA 4 : UNUNUZI NA UUZAJI WA BIDHAA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Mazungumzo

**Funzo**: Maamkizi na mazungumzo: Sehemu za uuzaji na ununuzi wa bidhaa

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kuzungumza akizingatia msamiati ufaao katika muktadha wa uuzaji na ununuzi wa bidhaa.
- Kuzungumza kwa mfululizo huku akizingatia matamshi bora na sarufi mwafaka.
- Kuandika mazungumzo katika muktadha wa uuzaji na ununuzi ya kiislamu kwa njia inayofaa.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Mazungumzo ni mafunzo yaliyopewa kipaumbele katika mtalaa huu wa Kiswahili. Sababu ni kuwa, mara nyingi watu huwasiliana kwa njia ya kuzungumza. Nayo mazungumzo hayo huathiriwa na mambo mengi kama vile dini, umri, rika, mazingira, mada, na kadhalika. Ni vyema mwanafunzi kufahamu na kujizoesha sajili mbalimbali ili aweze kukuza na kutumia msamiati na kaida zifaazo za mazungumzo. Wape wanafunzi nafasi ya kufanya mazoezi ya kuongea darasani huku ukiwaelekeza kuhusu msamiati, matamshi na kanuni nyingine muhimu kulingana na sajili inayohusika. Vilevile, ingefaa uwahimize kutumia Kiswahili nje ya darasa huku wakizingatia msamiati ufaao kulingana na sajili. Pia waelekeze kusoma tamthilia, riwaya na hata magazeti ya Kiswahili na baadaye uwaongoze kujadili matumizi ya lugha yaliyomo. Chukua siku mzuru maeneo mbalimbali ya kuuza na kununua bidhaa na waweze kuwasiliana na watu katika maeneo hayo katika Kiswahili. Itakuwa vyema iwapo ni maeneo yanayojua Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali kadha kuhusu mazungumzo katika muktadha wa Kiisilamu.
- Waagize wawili wao kuja mbele ya darasa na kuzungumzia suala fulani

linalohusu Uislamu huku ukiwapa mwongozo kuhusu msamiati ufaao katika muktadha huo.

- Waongoze kusoma mazungumzo yaliyomo kati ya Najma na Ahmed. Wachague wawili wawili kusoma huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji bora. Hakikisha kuwa wengi wao iwezekanavyo wamepata nafasi ya kusoma.
- Waite wawili wawili kuja mbele ya darasa wakiwa na vitabu vya kusoma na wajaribu kuigiza mazungumzo hayo huku ukiwapa maelekezo.
- Pitieni sehemu ya maelezo ya msamiati na pia mjadili maana za msamiati mwingine wasiouelewa.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo na kuwashauri vilivyo. Tathmini watakavyosoma mazungumzo hayo na kujibu maswali. Kuza mawasiliano na matamshi yao.

**Majibu**

1. Wanafunzi wataje msamiati wa biashara uliotumika katika kifungu mfano;duka la jumla,bidhaa,mteja,pauni,baki na kadhalika.
2. Muuzaji anaonyesha kujali mteja wake kwa kumsikiliza na kumtembeza amwonyeshe bidhaa.Anampa mwelekeo wa kila safu.
3. Ndiyo, tofauti ipo. Duka,mnunuzi anamwitisha muuzaji bidhaa. duka la jumla, mnunuzi anajichagulia bidhaa. Kwa wakati mwingi katikaduka la jumlabei huwa imebandikwa kwa bidhaa. Katika duka, mnunuzi husema bei.
4. Kupanga bidhaa katika duka humwezesha mteja kuchagua kwa urahisi anachotaka,uzuia bidhaa kuchanganyika.
5. Kuandika orodha ya bidhaa utakazonunua husaidia mteja asisahau bidhaa nyingine.

## KUSOMA

### ADABU KATIKA MAENEO YA MAUZO

**Funzo**: Ufahamu - Adabu katika maeneo ya mauzo

**Malengo maalum**: Baada ya funzo mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na barua iliyomo.
- Kutaja sababu mbalimbali zinazowafanya wanafunzi kushiriki migomoni na jinsi ya kuepukana na hali hizi.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na adabu na heshima katika sehemu za mauzo, kwa mfano:
  a) Bidhaa zinazouzwa ni za nani?
  b) Je, mteja ana uhuru wa kushika vitu katika sehemu za mauzo bila idhini?
  c) Je, kama ni vitu hatari, mteja anafaa kufanya nini kabla ya kugusa bidhaa hiyo
  d) Je, ni vyema mteja kuruhusu watoto wake kucheza na bidhaa za muuzaji?
  e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa ili kupunguza migomo shuleni?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Majibu**

1. Vibanda,duka,duka la jumlana au soko
2. Kupanga bidhaa vizuri,kuimbia bei,kuvalia mavazi ya kuvutia mteja, mfano, mwanamume kuvaa rinda.
3. Huonyesha kuwajibika kwa mteja na pia kuna sheria za kila bidhaa.
4. Huenda ukauziwa kwa bei ya kupunguza gharama.

5. Kukosa nafasi kubwa hadharani ya kuweka bidhaa zote; pia bidhaa nyingine zinakingwa kutokana na vumbi na uchafu.
6. Ikiwa pesa zako zinazidi bei ya bidhaa.
7. Kutoka kwa kinachouzwa.
8. Ndio,ikiwa atauza bidhaa kwa bei ya chini kuliko alivyonunua auunapomrudishia mnunuzi baki nyingi kuliko iliyotarajiwa.Bidhaa zinavunjwa au kuharibiwa.
9. Kutoharibu au kapaka uchafu bidhaa kama hizi. Nyingine zilezinazoweza kuvunjika zinahitaji kukaguliwa kwa uangalifu.
10. Maana ya maneno haya ni:
    i. bidhaa -vitu vinavyouzwa
    ii. bei -kiwango kwa malipo kilichowekewa bidhaa fulani
    iii. kwenda hasara -kupoteza faida ya bidhaa
    iv. baki -Pesa za juu anazorudishiwa mteja ikiwa alipeana zaidi

## SARUFI

Umoja na Wingi wa Nomino

**Funzo I.**: Umoja na wingi wa nomino

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua nomino katika hali ya umoja na wingi.
- Kubainisha wingi wa nomino.
- Kupatanisha nomino za Kiswahili na maneno mengine yaliyotumika kwenye tungo.
- Kuandika nomino katika umoja na wingi.
- Kujibu maswali yaliyomo kwa njia sahihi.

**Vifaa**

Chati yenye nomino katika umoja na wingi na chati yenye ngeli za nomino kulingana na kigezo cha upatanisho wa kisarufi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kufikia sasa wanafunzi wameshajifunza mengi kuhusu nomino. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hayo. Vilevile, wape nafasi ya

kubainisha matumizi ya ngeli mbalimbali kimuktadha hasa kutokana na vitabu vya ziada. Kujua wingi na umoja wa nomino utwapa msingi bora wa ngeli na kama tujuavyo ngeli ndio msingi wa sarufi, na kwa hivyo ni muhimu sana wanafunzi kuzielewa na kuzitumia katika miktadha mbalimbali, sio tu darasani lakini hata nje ya darasa.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu nomino kama vile:
  a) Nomino ni nini?
  b) Ni nini umuhimu wa nomino katika mawasiliano?
  c) Nini wingi wa nomino ‘mwanafunzi’
  d) Nomino ‘mwanafunzi’ imo katika ngeli gani kulingana utaratibu wa upatanisho wa kisarufi?
  e) Taja ngeli mbalimbali za Kiswahili, na kadhalika.
- Waelekeze wanafunzi kusoma maelezo na ufafanuzi uliomo kitabuni. Waweza kuwapa nafasi ya kusoma mmoja mmoja kwa sauti huku ukiwafafanulia zaidi na kuwapa mifano ya ziada. Pia waulize maswali katika kila hatua. Unaweza kuwaagiza kuandika baadhi ya majibu unayowauliza ubaoni ili jambo hili liwe chanzo cha mjadala darasani. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada. Hakikisha umeyasahihisha na kuwashauri. Pia endelea kuwapa moyo huku ukiwaonyesha kwamba kuelewa ngeli ni jambo rahisi sana mradi tu mtu afahamu kanuni zinazotumika katika kuziratibu.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwashauriipasavyo.

**Majibu**

a) Wanafunzi wajaze mraba katika umoja na wingi wa nomino

| Nomino kwa umoja | Nomino kwa Wingi |
|---|---|
| 1. mteja | **wateja** |
| 2. **kipimo** | vipimo |
| 3. chumvi | **chumvi** |

| | |
|---|---|
| 4. **sukari** | sukari |
| 5. kinywaji | **vinywaji** |
| 6. **mafuta** | mafuta |
| 7. chupa | **chupa** |
| 8. **pesa** | pesa |
| 9. tunda | **matunda** |
| 10.**mboga** | mboga |
| 11.bidhaa | **bidhaa** |
| 11. **mnunuzi** | wanunuzi |
| 12. duka | **maduka** |
| 13. **mkate** | mikate |
| 14. muuzaji | **wauzaji** |
| 15. **sukari** | sukari |
| 16. unga | **unga** |
| 17. **kitanda** | vitanda |
| 18. runinga | **runinga** |
| 19. **mkunguwa ndizi** | mikungu ya ndizi |
| | |

**b)**

1. _____ anauza vitu **(Muuzaji,**Mnunuzi)
**2.** Nyumba kubwa ya kuuzia vitu ni _____. (kibanda,**duka)**
3. Vitu vinavyouzwa huitwa _____. (**bidhaa**,mteja)
4. _____ ni kubalishana pesa na vitu. **(Kuuza**,kulinda)
5. Mtu ananunua vitu dukani huitwa _____. **(mteja**, kashia)
6. Pesa ambazo vitu hununuliwa huitwa _____. (mabaki,**bei)**
**7.** _______ni pesa za juu anazopata muuzaji.(Hasara**, Faida)**
8. Pesa za juu anazorudishiwa mtu baada ya kununua vitu huitwa _____. (**baki,**hasara)
9. _____ ni vitu anavyonunua mtu.(Vipimo, **Bidhaa**)

10. Muuzaji asipozingatia pesa kamili za bidhaa anapata **_____**. (**hasara**,faida)

**c) Kuandika sentensi katika wingi**

i. Mikate iliyookwa ni mitamu.
ii. Wanunuzi walirudisha bidhaa.
iii. Maji ya chupa si mazuri.
iv. Wauzaji walipata hasara jana.
v. Maboga yatanunuliwa jioni.
vi. Wanafunzi wasiuziwe vinywaji vya kulevya.
vii. Wateja waliuliza vipimo vya bidhaa.
viii. Vibanda vilibolewa juzi.
ix. Maduka makubwa yalihamishwa pale.
x. Mabaki waliyopewa yalipotelea njiani.

## Aina za nomino

**Funzo II.**: Aina za nomino

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kufafanua maana ya nomino.
- Kutambua aina za nomino.
- Kutumia aina mbalimbali za nomino kwa usahihi.
- Kujibu maswali yaliyomo kwa njia sahihi.

**Vifaa**
Chati yenye nomino mbalimbali

**Mawaidha kwa mwalimu**
Kufikia sasa wanafunzi wamejifunza mengi kuhusu nomino. Wajibu wako ni kuzidi kuwapa mawaidha, mazoezi na maelekezo zaidi. Jaribu kutumia vifaa mbalimbali vya kufundishia unapofanya hayo. Vilevile, wape nafasi ya kubainisha nomino mbalimbali kimuktadha hasa kutokana na vitabu vya ziada na vya fasihi. Ngeli ni msingi wa sarufi na, kwa hivyo, ni muhimu sana wanafunzi kuzielewa nomino na aina zake na kuzitumia katika miktadha mbalimbali, si tu darasani lakini hata nje ya darasa.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu nomino kama vile:
  a) Nomino ni nini?
  b) Taja nomino unazojua.
  c) Kuna aina ngapi za nomino?
  d) Je, unaweza kutumia nomino katika sentensi?
  e) Neno ‘kondoo’ ni aina gani ya nomino?
- Waelekeze wanafunzi kusoma maelezo na ufafanuzi uliomo kitabuni. Waweza kuwapa nafasi ya kusoma mmoja mmoja kwa sauti huku ukiwafafanulia zaidi na kuwapa mifano ya ziada. Pia waulize maswali katika kila hatua. Unaweza kuwaagiza kuandika baadhi ya majibu unayowauliza ubaoni ili jambo hili liwe chanzo cha mjadala darasani. Unaweza kuwapa wanafunzi ambao wanatatizika zaidi katika weledi wa funzo hili ufafanuzi zaidi wakiwa mmoja mmoja na hata mazoezi ya ziada. Hakikisha umeyasahihisha na kuwashauri. Pia endelea kuwapa moyo huku ukiwaonyesha kwamba kuelewa ngeli ni jambo rahisi sana mradi tu mtu afahamu kanuni zinazotumika katika kuziratibu.

**Tathmini**

Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na

Kuwashauri ipasavyo.

**Majibu**

a) Kupigia mstari nomino katika sentensi zifuatazo:

i. Dadayangu alienda.
ii. Wananchi wote watatembea.
iii. Kila mwanafunzi ni lazima asome.
iv. Bidhaazake zimeoza.
v. Nilimuuliza aniuzievitu vyote.
vi. Mashamba yao yalinyakuliwa.
vii. Watamtembelea mteja wao .
viii. Masomo yakutahiniwa yalipunguzwa.
ix. Mchuuzi alizurura sana.
x. Pesa alizokuwa nazo hazitoshi.

**b) Kutambua nomino katika sentensi na kutaja ni ya aina gani**

i. Kusoma kuna manufaa mengi - **nomino ya kitenzi-jina**
ii. Mto Tana ulifurika mvua iliponyesha.- **nomino halisi/pekee/maalum**
iii. Khamisi alinibebea nilipoumia. - **nomino halisi**
iv. Dini yetu inahimiza kusaidiana. - **nomino ya kawaida**
v. Utukutu wake ulimuathiri sana. **-** **nomino ya dhahania**
vi. Mwanaishaanapenda kusoma. - **nomino halisi/pekee/maalum**
vii. Jumamosi ni siku ya kupumzika.- **nomino halisi/pekee/maalum**
viii. Vitabu vya kusoma vimenunuliwa. - **nomino ya kawaida**
ix. Muuzajialinidai nilipomlipa. - **nomino ya kawaida**.
x. Maji yakimwagika hayazoleki. - **nomino ya wingi**

1. Kutambua aina za nomino katika sentensi
   **i.** Mama alininunulia maziwa. (**kawaida)**
   ii. Walipoenda kwao walimkuta akila nyama**. (kawaida)**
   **iii.** Mlima kilimanjaroni mkubwa .(**halisi)**
   **iv.** **Uvivu** wake utamwangamiza. (**dhahania)**
   **v.** **Maziwa**yote yalimwagika. (**ya wingi)**
   **vi.** Mtoto alipongezwa kwa **bidii** masomoni. (**dhahania).**
   **vii.** **Seremala Juma** alitengeneza viti. (**halisi)**
   **viii.** **Umati wa watu** ulimzunguka mwalimu mkuu. (**kundi)**
   **ix.** Barabara ilijaa **matope** mengi. (**kawaida)**
   **x.** Nyimbo za **Desemba** zimetungwa**. (halisi)**

## Wakati Uliopo, Wakati Uliopita na Ukanusho

**Funzo**: Nyakati na ukanusho.

**Malengo maalum:** Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kutambua nyakati zilizofunwa
- Kutumia nyakati zilizofunwa
- Kukanusha nyakati mbalimbali
- Kujibu maswali kwa usahihi.

**Mawaidha kwa mwalimu**
Kukanusha vitenzi ni funzo linalofaa kutiliwa uzito mwingi kwa sababu ni kipengele muhimu sana katika sarufi ya Kiswahili. Hata hivyo, funzo hili huonekana gumu kwa wanafunzi iwapo halitashughulikiwa kwa njia inayofaa. Kwa sababu, wanafunzi hulikanganya na kinyume cha vitenzi. Wanafunzi wanastahili kujua kuwa kukanusha ni kukataa kutukia kwa kitendo Kwa hivyo, utahitaji kuchukua muda zaidi unapolishughulikia kuwapa ufafanuzi na mazoezi ya kutosha. Vilevile, wape mazoezi ya ziada kutokana na vitabu vya fasihi, magazeti na hata majarida.

**Utaratibu**
- Waongoze wanafunzi kupitia maelezo yaliyomo kitabuni huku ukiwapa ufafanuzi na mifano zaidi.
- Katika kila hatua, waagize wanafunzi kutoa mifano zaidi huku mkiijadili.
- Chagua wanafunzi wawili wawili, mmoja wa atunge sentensi na mwingine wa akanushe sentensi hizo.

**Tathmini**
Wape wanafunzi zoezi lifuatalo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri yafaayo:
Ukifuata mfano ufuatao, kamilisha sentensi zifuatazo, k.m:

Mlango ulifunguka wenyewe.

Mlango haukufunguka wenyewe.

1. Baba alifunga mlango.
2. Nitapika chakula.
3. Dada yangu alisoma vizuri.
4. Mimi nilipakua chakula kingi.
5. Chakula hiki kinanuka.

Wape wanafunzi muda wa kufanya zoezi katika kitabu
**Majibu**

a) Kuchagua sentensi zilizotumia **wakati uliopita** pekee
   i. Rais aliwahutubia wananchi waliomngonjea.
   ii. Basi la shule lilisafirisha wanafunzi walioathirika.

iii. Ugonjwa wa UKIMWI ulimuua mtoto alipolala.
iv. Bidhaa ziliuzwa kibandani mlimokuwa mnaishi.
v. Tulijadiliana bei na mteja aliyetaka kununua shamba.
vi. Mbwa mkali alimfukunza mtoto aliyemkaribia.
vii. Polisi waliwatuliza vijana waliotaka kumchoma mwizi.

b) Mwalimu, hakiki sentensi walizotunga wanafunzi katika wakati uliopo.

c) Kukanusha sentensi

i. Babu yangu hakunifunza kuheshimu watu.
ii. Kuku wa jirani hakuliwa na mbwamwitu.
iii. Sikuhudhuria arusi yake huko kijijini.
iv. Nguo za mtumba hazina bei nafuu.
v. Meli ya tatu haibebi mizigo yote.

## KUANDIKA

### Barua rasmi

**Funzo**: Utungaji wa kiuamilifu – Barua rasmi

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza muundo wa barua rasmi.
- Kueleza sifa za barua rasmi
- Kuandika barua rasmi kwa njia inayofaa.

**Majibu:**

1. Aliyeiandika barua ni Mwanaisha Abubakar.
2. Aliyeandikiwa barua hii ni Mkurugenzi, wa Kampuni ya LITZO iliyoko Kitengela.
3. Sababu za kuiandika barua hii kulalamika juu ya mashine ghushi, zilizowasilishwa katika duka la Mwanaisha Abubakar.
4. Mwandishi analalamikia kupokezwa Mashine za kizamani sana na zilizopitwa na wakati. Pia Mashine hizi hazina mhuri wa Kampuni ya Litzo.

**Vifaa**

Barua rasmi mbalimbali, chati ya barua rasmi

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali kuhusu umuhimu wa urasmi.
- Ukitumia barua rasmi mbalimbali, wafafanulie namna zinavyoandikwa.
- Waambie wakueleze sababu za kuandika rasmi za aina mbalimbali.
- Waongoze kupitia ufafanuzi uliomo huku ukiwapa mifano zaidi.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri zaidi. Wazingatie muundo wa barua rasmi bila kusahau ujumbe.

# SURA YA 5 : AFYA NA MAGONJWA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Shairi

**Funzo**: Kukariri shairi

**Malengo maalum**: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kusikiliza kwa makini
- Kukuza msamiati wake.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na kusikiliza kwa makini na kutamka maneno kwa usahihi. Vile tulivyosema hapo awali, buni mbinu mbalimbali za kukuza matamshi hata ikiwa ni nyimbo, mijadala, mazungumzo na hotuba. Kukuza kipawa cha kuzungumza hadharani na kutamka kwa usahihi maneno na silabi ni jambo muhimu sana. Hili huwapa wanafunzi ujasiri mno. Vilevile, kutilia mkazo, shadda, kiimbo na toni. Kwa hivyo, mashairi na nyimbo kama sanaa vitawawezesha kuchangamkia Kiswahili na hiyo itakuwa hatua nzuri katika kufunza na kuwahamasisha kuhusu lugha hii. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa unakariri na kutamka maneno kwa ufasaha mno. Zingatia shadda na kiimbo. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
    d) Nani atakariri shairi?
    e) Nani atatutajia sifa za shairi?

f) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?

- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaohusu na usafi na jinsi ya kujitunza.

**Majibu**

1. Watu wasiogope kwenda kupimwa
2. Anamaanisha ni heri mtu apimwe na ajue hali yakemapema kuliko kuja kujua ugonjwa dakika za mwisho.
3. Ili waishi kwa furaha.
4. Kina baba,kina mama,vongozi na watoto
5. Maana ya ndani ni kuwa

i. Madhara hayavumiliki

ii. watu waepuke madhara ya magonjwa mapema.

## KUSOMA

### MISINGI YA KUWA NA AFYA NJEMA

**Funzo**: Ufahamu – Misingi ya kuwa na afya njema

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali kwa usahihi.
- Kuishi kwa afya na amani.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na adabu na heshima katika sehemu za mauzo, kwa mfano:

a) Bidhaa zinazouzwa ni za nani?

b) Je, mteja ana uhuru wa kushika vitu katika sehemu za mauzo bila idhini?

c) Je, kama ni vitu hatari, mteja anafaa kufanya nini kabla ya kugusa bidhaa hiyo

d) Je, ni vyema mteja kuruhusu watoto wake kucheza na bidhaa za muuzaji?

e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa ili kupunguza migomo shuleni?

- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Majibu**

1. Vyakula vinajenga mwili na kuukinga dhidi ya uvamizi wa virusi vyovyote
2. Maji husaidia wepesi wa kusaga na kusafirisha chakula mwilini.
3.Kisukari, presha, moyo
4. i. Mazoezi husaidia vishimo vidogo vilivyoko kwenye ngozi kufunguka na kupata hewa safi,husaidia usafirishaji wa damu kwenye mishipa,huchoma mafuta yaliyokwamia mishipani.

ii.Ugonjwa wa presha huletwa na msongo au fikira nyingina mbinu za kukabiliana na mawazo mengi maishani ni kwa kufanya mazoezi ya mwili, kuimba,kucheka na wenzako,kuangalia filamu nzuri au kuingia kwenye miradi itakayo kuondolea fikira.

iii. Tuweze kubainisha dalili za magonjwa,

iv. Tusome,kusikiliza na kuhudhuria mikutano inayofunza juu ya afya.

v. Tutunze mili kwa kuijali.

**Shughuli ya ziada**

**MALARIA NA KIFUAKIKUU**

**Funzo** : Ufahamu – Malaria na kifua kikuu

**Malengo maalum** : Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na ufahamu.

- Kutaja sababu mbalimbali zinazofanya watu kuugua malaria.
- Kutaja mbinu za kujikinga na malaria.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na magonjwa, kwa mfano:
  a) Magonjwa ni nini?
  b) Kuna magonjwa gani?
  c) Taja magonjwa hatari na sababu za magonjwa hayo kuwa hatari.
  d) Je, unajua malaria?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja asome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Tanbihi: Hii ni kazi ya ziada kwa wanafunzi. Wasome na kuimarisha maarifa yao kuhusu magonjwa ya malaria na kifuakikuu**

**Majibu**

1. Malaria na kifuakikuu.
2. Njia za kuambukizwa magonjwa ya:
   a) Malaria-kuumwa na mbu wa kike aliye na viini vya malaria.
   b) Kifuu kikuu-kupitia kwa bakteriayenye viini hivi.
3. Dalili za;
   a) Malaria-homa, kuhisi baridi, kutokwa na jasho, maumivu ya kichwa na mwili, kichefuchefu, na kutapika, kuhisi joto kali, kutetemeka kwa mwili,maumivu ya misuli na kuendesha.
   b) Kifuukikuu- Kikohozi cha muda mrefu kama wiki mbili au zaidi,kukohoa damu,homa isiyoisha;hasa homa ambayo inapanda

sana wakati wa usiku; ikiambatana na kutoka jasho jingi wakati wa usiku kiasi cha kulowesha mashuka,kupungua uzito kusiko kawaida na pia maumivu ya kifua wakati wa kukohoa,kupungua hamu ya kula,kuchoka na kutoka jasho wakatiwa usiku.

4. Njia za kujinga kuambukizwa Malaria ni pamoja na kutumia chandarua kilichowekwa dawa ya kuua mbu na kisiwe na shimo au tundu; kupuliza dawa ya kuua wadudu nyumbani mwako; kuweka wavu wa kuzuia wadudu katika madirisha na milango;kutumia kiyoyozi na feni ili kufukuza mbu; kuvaa nguo zenye rangi angavu na zinazofunika mwili vizuri; kuepuka kuwa katika maeneo yenye mbu wengi, mabwawa yenye mbu, na maji yaliyotuama, mahali ambapo mbu huzaliana.
5. Ndio, kutumia dawa zisizofaa au dawa bandia kunaweza kuzidisha ugonjwa na kuhatarisha uhai.
6. Kuondoa vitu vyovyote vinavyozunguka nyumba kama vile mikebe, chupa na mitungi wazi vinavyoweza kuchangia mbu kuzaliana.
7. Pata habari za karibuni kuhusu ugonjwa huo kwani aina ya vimelea vya malaria wa eneo moja huenda vikatofautiana na vya eneo jingine, jambo hilo litakusaidia kuamua aina ya dawa inayofaa zaidi.
8. Bakteria ya kifua kikuu inaathirikwenye mapafu, figo, katika utumbo wa chakula, ngozi, ubongo na kwingineko.
9. Kutokana na kuishi au kuwa karibu na mtu mwenye ugonjwa huo na mara anapopiga chafya au kukohoa bila kufunika mdomo ndipo wadudu hao wanaweza kukuambukiza.
10. Ndio, kula vyakula visivyopikwa vikaiva kama kunywa maziwa ambayo hayajachemshwa kuna hatari ya kupata bakteria hao.
11. Wale wanaoishi kwa karibu na kwa muda mrefu na mtu yule aliyekwisha kuambukizwa ugonjwa huo na ambaye bado hajaanza matibabu;watoto wadogo na wazee; wale wote wanaougua kisukari; watu wanaotumia dawa zinazoathiri mfumo wa kinga ya mwili; waathirika wa ukimwi; wale wote wanaoishi maeneo yenye msongamano mkubwa watu wanaoishi kwenye sehemu zisizokuwa na hewa ya kutosha; watu wanaotumia dawa mbalimbali au pombe na mwisho walewenye lishe duni.
12. Hakikisha unapokohoa au kupiga chafya unafunika mdomo wako pia unapotema mate hakikisha unayafukia vizuri.

13. Kujihakikishia afya yako na kuanza tiba mapema kabla ilmuradi usiwaambukize watu wengine.
14. Dalili ambazo ni sawa kwa mtu mwenye malaria na yule mwenye kifua kikuu nihoma kali,kutokwa na jasho najoto
15. Mwalimu, hakiki sentensi za wanafunzi.

**Shughuli ya ziada 2**

## UKIMWI

**Funzo**: Ufahamu – UKIMWI

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na UKIMWI.
- Kutaja mbinu za kuambukiza na kujikinga UKIMWI.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodosokuhusiana na magonjwa, kwa mfano:
  a) Unajua magonjwa gani?
  b) Ugonjwa gani hatari sana?
  c) Je, kuna mbinu gani za kujikinga na magonjwa hayo?
  d) Je, watu wagonjwa wanaathiri vipi jamii na uchumi?
  e) Je, UKIMWI ni ugonjwa gani?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Tanbihi:** Hii ni kazi ya ziada kwa wanafunzi. Wasome na kuimarisha maarifa yao kuhusu UKIMWI.

**Majibu**

1. Kumnasa panya.
2. Hawakuwa na uwezo wa kuondoa ule mtego.
3. Kuku,ng'ombe na mbuzi.
4. Waliohudhuria mazishi walikuwa wengi na walihitaji mboga nyingi.
5. Kisa hiki kinatufunza kuwa ugonjwa wa UKIMWI unaweza kuathiri yeyote na tusiwabague walioathiriwa.

**Shughuli ya ziada 3**
**KANSA**

**Funzo**: Ufahamu – Kansa

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na UKIMWI.
- Kutaja mbinu za kuambukiza na kujikinga UKIMWI.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodosokuhusiana na magonjwa, kwa mfano:
  - f) Unajua magonjwa gani?
  - g) Ugonjwa gani hatari sana?
  - h) Je, kuna mbinu gani za kujikinga na magonjwa hayo?
  - i) Je, watu wagonjwa wanaathiri vipi jamii na uchumi?
  - j) Je, kansa ni ugonjwa gani?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.

- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**
Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Tanbihi:** Hii ni kazi ya ziada kwa wanafunzi. Wasome na kuimarisha maarifa yao kuhusu kansa.

**Majibu**

1. Saratani
2. Seli za mwili zikizeeka hufa lakini seli za kansa huendelea na kuzaana.
3. Ndio, hukua sana na kuvibana viungo na tishu nyingine mwilini.
4. Ukuaji wa seli usiodhibitika, uwezo wa kuvamia na kushambulia tishunyingine na uwezo wa kusambaa katika viungo vingine mwilini kupitia mishipa ya damu.
5. Kansa ambayo inawapata :
    a) Kina mama-ya matiti
    b) Watoto-ya damu
6. Nyama nyekundu, nyama zilizosindikwa, vyakula vilivyokuzwa kwa kemikali nyingi kama mbolea, vyakula vyenye mafuta mengi,vyakula vilivyoota ukungu, kwa mfano, karanga nyama zilizosindikwa pamoja na zile zilizohifadhiwa kwa kuongezwa chumvi, mafuta, kemikali au kukaushwa.
7. Sukari inachangia katika ukuaji wa seli za kansa.
8. Ndio,ikitambulikana mapema na mwathiriwa akienda kwa matibabu.
9. Nafaka zisizokobolewa kama vile unga wa ngano usiokobolewa sana, unga wa dona, mchele wa brauni, ulezi na aina mbalimbali za mikunde kama vile maharage, kunde, choroko na mbaazi.
10. Kukojoa mara nyingi zaidi ya kawaida au mkojo kutoka kwa shida; uvimbe wa zaidi ya wiki tatu shingoni, kwapani, tumboni, ngozi au matiti; kubadilika kwa kawaida ya kupata choo (kufunga choo); matiti kubadilika umbile, uvimbe, ngozi au kutoa maji maji;kukohoa au sauti ya

kukwaruza kwa zaidi ya wiki tatu; shida au maumivu wakati wa kumeza chakula au vinywaji; kutokwa na damu kwenye choo, mkojo, makohozi au pua; uchovu bila kufanya kazi; kupungua uzito ghafla bila sababu na kukosa hamu ya kula chakula.

## KUANDIKA

**Funzo**: Insha ya mazungumzo.

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza maana ya insha ya mazungumzo.
- Kutaja sifa za insha ya mazungumzo.
- Kuandika insha nzuri ya mazungumzo.

**Utaratibu**

- Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya dodoso kuhusu uandishi wa insha kwa jumla, kwa mfano:
  a) Insha ni nini?
  b) Ni mambo gani yanayofaa kuzingatiwa katika uandishi wa insha?
  c) Insha ya mazungumzo ina sifa zipi?
- Waelekeze kusoma kimya mazungumzo katika magazeti na majarida. Kisha, chagua wawili wa kusoma nafasi za wahusika huku mwingine mmoja akisoma maelezo mabanoni. Wasome kwa sauti huku ukiwaelekeza kuhusu usomaji ufaao hasa wa matamshi, sarufi, kiimbo na kadhalika.

**Tathmini**

- Waelekeze wanafunzi kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri zaidi.
- Hakikisha kuwa wanafunzi wameandika insha hii ya mazungumzo. Isahihishe na kuwashauri vilivyo.
- Tilia maanani hati ya mwanafunzi. Maumbo ya herufi ni muhimu katika kuandika insha.
- Hakikisha:

1. Mwanafunzi ameandika mazungumzo baina ya mgonjwa na daktari.
2. Mwanafunzi ameandika mawasiliano yake na mhudumu wa ambulensi yakuwaokoa.

# SURA YA 6 : MILA, UTAMADUNI NA ITIKADI

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### Shairi

**Funzo 1**: Kukariri shairi–Tulisahau utamaduni wetu lini

**Malengo maalum**: Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

- Kutaja sifa za mashairi.
- Kuchangamkia mashairi.
- Kutamka maneno kwa usahihi.
- Kukariri shairi.
- Kutumia msamiati wa ushairi kwa usahihi.

**Mawaidha kwa mwalimu**
Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na sifa na tofauti baina ya mashairi ya arudhi na yale huru – mbona hili liitwe la 'huru' na linalofuata (2) 'arudhi'? Pia elewa kuwa wanafunzi wengi huamini kuwa mashairi ni sanaa ngumu inayotaka 'malenga' pekee. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Waeleze na kuwaonyesha arudhi: mizani, vina, muwala na utoshelezi kwa jumla. Waeleze pia kuhusu matumizi ya uhuru wa mwandishi huku ukiwaonyesha mpaka wa uhuru huo ili wasiboronge lugha kiholela wakidhani wanatumia 'uhuru'. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa umewatungia shairi fupi la kuwatolea mfano. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**
- Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
  - a) Taja kwa jumla, sifa za mashairi.
  - b) Ni vipengele gani muhimu unavyopaswa kuzingatia katika kukariri shairi?
  - c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?

- Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu mazingira na utunzi wake.

**Tathmini**

- Waelekeze wanafunzi katika kujibu maswali waliyoagizwa. Unaposahihisha ona kuwa silabi na maneno yameandikwa kuzingatia sarufi wala si kuboronga jinsi ilivyo katika shairi.
- Mwanafunzi atumie lugha ya kinathari kujibu maswali huku akizingatia ujumbe.

**Majibu**

1. Lawama za mshairi kwa wafuatao:
    a) Kina mama-wanafanya mapenzi na watoto wao
    b) Wasichana-wanavaa mini-sketi,hawavai chupi,wanafanya mapenzi na mababa zao,washerati,wanaavya mimba.
    c) Kina nyanya-wanapapasapapasa vijana na kuwaweka unyumba
2. Kupapasapapasana mabintizao, na uzininifu
3. Ndio, misikiti imegeuka soko,makanisa yamebadilikakuwa madanguro,uzinifu unafanywa huko.
4. Kuishi kama mke na mume bila kuoana.
5. Ili wafanye usherati na yeyote.
6. Kuoa bila idhini ya wazazi,kuwafokea wazazi,kuketi wazee wakiwa wamesimama; kuwekwa unyumba
7. Maana ya:
    a) yawapwaya-yanayoning'inia
    b) chupi-suruali ya ndani ya mwanamke
    c) mahaba-mapenzi
    d) bughudha-maneno ya kuudhi
    e) kufokea-kumwongelesha mtu kwa kumwamrisha

## Kukariri shairi

**Funzo 2** : Kukariri shairi – Utamaduni wa kweli

**Malengo maalum** : Kufikia mwisho wa kipindi, mwanafunzi aweze:

-  Kutaja sifa za mashairi.
-  Kuchangamkia mashairi.
-  Kutamka maneno kwa usahihi.
-  Kukariri shairi.
-  Kutumia msamiati wa ushairi kwa usahihi.

**Mawaidha kwa mwalimu**

Kuna haja ya wanafunzi kutanzukiwa kikamilifu na sifa na tofauti baina ya mashairi ya arudhi na yale huru – mbona hili liitwe la arudhi' na lile la awali (1) huru'? Pia elewa kuwa wanafunzi wengi huamini kuwa mashairi ni sanaa ngumu inayotaka 'malenga' pekee. Waonyeshe urahisi na uzuri wa kukariri mashairi na jinsi wao pia waweza kuwa manju. Waeleze na kuwaonyesha arudhi: mizani, vina, muwala na utoshelezi kwa jumla. Waeleze pia kuhusu matumizi ya uhuru wa mwandishi huku ukiwaonyesha mpaka wa uhuru huo ili wasiboronge lugha kiholela wakidhani wanatumia 'uhuru'. Hili litawezekana endapo wewe mwenyewe utakuwa umewatungia shairi fupi la kuwatolea mfano. Wakaririe shairi kwa mahadhi ya kupendeza ili kuwachangamsha na kuwavutia kutaka kukariri kama wewe. Mbinu hiyo itarahisisha matamshi yao na kufanya wapende kuzungumza na kusikiliza Kiswahili.

**Utaratibu**

-  Anza kwa kuwauliza maswali ya kuwadodosa kama vile:
  a) Taja kwa jumla, sifa za mashairi.
  b) Ni vipengele gani muhimu unavyopaswa kuzingatia katika kukariri shairi?
  c) Je, mashairi yana umuhimu gani kwa mpenzi wa Kiswahili?
-  Huku mkirejelea shairi lililo katika Kitabu cha Mwanafunzi, wakaririe kikamilifu shairi hilo. Kariri nao pamoja ili kuwapa ukakamavu na ujasiri. Waulize msamiati unaopatikana katika shairi unaousu mazingira na utunzi wake.

**Tathmini**

-  Waelekeze wanafunzi katika kujibu maswali waliyoagizwa. Unaposahihisha

ona kuwa silabi na maneno yameandikwa kuzingatia sarufi wala si kuboronga jinsi ilivyo katika shairi.

- Mwanafunzi atumie lugha ya kinathari kujibu maswali huku akizingatia ujumbe.

**Majibu**

1. i. Watoto wadogo kuozwa; ukeketaji
   ii. Kuna ubakaji,usherati namapenzi ya lazima
   iii. Haki ya elimu na malezi bora
   iv. Maana fiche ya maneno haya:
      i. Michezo ya baba na mama- ngono.
      ii. Vitu vyenye ncha kali-kuchezea mapenzi
      iii. Sindano za mitaa-wanaoharibu watu kimapenzi

# KUSOMA

## MILA NA UTAMADUNI

**Funzo**: Ufahamu – Mila na utamaduni

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali yanayotokana na barua iliyomo.
- Kutaja mila, tamaduni na itikadi za jamii yake.
- Kujua mila, tamaduni na itikadi nzuri na mbaya katika jamii yake

**Marejeleo**

Kitabu cha Mwanafunzi (Uk. 70-73).

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na madabu na heshima katika sehemu za mauzo, kwa mfano:
  a) Mila ni ninii?
  b) Utamaduni ni nini?

c) Je, kuna mila na utamaduni nzuri na mbaya?
d) Je, mnashiriki na kuendeleza mila na tamaduni za aina gani?
e) Je, ni vyema kushiriki katika mila na tamaduni zinazokandamiza?
f) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa ili kupunguza mila kandamizi?

- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye, chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Majibu**

1. Ni vitendo ambavyo jamii fulani inashikilia lakini vina madhara kwa watu wake.
2. Kuvuja damu mpaka kufa na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kwa sababu ya kutumia kisu kimoja.
3. Wanawake wanaoozwa wanaume wanakaa maisha ya dhiki na vitisho.
4. Huwa hakuna mapenzi bali ni shinikizo kutoka kwa jamii.Pili kuna ugonjwa wa UKIMWI.
5. mama anampa mtoto wa kike kazi nyingi huku mtoto wa kiume amestarehe
6. Hafanyi kazi.Anastarehe na pengine kutazama runinga au kulala.
7. Mahitaji yanaongezeka; ugonjwa wa UKIMWI kwa kushiriki kitendo cha ndoa na wenzi wengi; hatari ya kupatwa na saratani ya sehemu za uzazi na magonjwa ya zinaa.
8. Mtu anaweza kuonekana mwenye afya,kumbe ameathiriwa na UKIMWI na anameza dawa akiwa amejificha.
9. Kupata idhini ya wazee kabla ya kuoa; kumtambulisha mchumba wako kwa walezi wako kabla ya kuoana; kuheshimu mahali kunakochukuliwa kuwa kutakatifu na kuita mikutano ya wazee ya kusuluhisha mambo kadhaa katika jamii.

10. Mwanafunzi ataje ikiwa kuna mila na utamaduni unaopaswa kusahaulika katika jamii yake na aeleze kwa nini.

## JAMII ZETU

**Funzo 2**: Ufahamu – Jamii zetu

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali kwa usahihi.
- Kutambua jamii zinazomzunguka
- Kujua mila, tamaduni na itikadi muhimu katika jamii yake.
- Kutathmini mila, tamaduni na itikadi za jamii mbalimbali.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na jamii mbalimbali wanazozijua, kwa mfano:
  a) Taja jamii unazozijua.
  b) Kuna tofauti gani kati ya jamii yako na ya mwingine?
  c) Je, mila zipi ni hatari katika jamii?
  d) Je, mila zipi zinaendeleza jamii?
  e) Ni hatua zipi zinazofaa kuchukuliwa ili kukuza mila na itikadi zetu?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Majibu**

1. Ni imani na mienendo ya watu wa jamii fulani katika shughuli zao za kila siku.
2. “Watu wa watu”
3. Ni njia ya kutambulisha na urembo kwa wanawake wao.
4. Mwanamke kutopata watoto.
5. Mvulana hatarajiwi kushinda akimtembelea msichana pasi kuwa na marafiki wake au hata watu wa jamii yake; kuchumbiana kunapaswa kuwa katika makazi ya msichana tu na si kwingine; mvulana kuhitajika kulipa mahari ya kiwango cha juu.
6. Mtu hutambulikana kutokana na idadi ya mifugo aliyonayo. Heshima na urithi wa mtu wa Wadinka hutegemea mifugo aliyonayo.Mifugo hutumika kulipia mahari.
7. i. Wadinka na Wanuer ambao ni wavuvi,wakulima na wawindaji,hufuga mifugo kwa idadi kubwa.

   ii. Kabila la Wadholuo ni wafugaji wadogo wa ng’ombe pamoja na ufagaji mkubwa wa kondoo na mbuzi na ni wavuvi.

   iv. Washilluk na Waaynuak ni wawindaji mashuhuri.

   v. Wazande ni wakulima na wasusi wa vikapu,meza,viti,nyuta,mishale na kofia kutoka kwa matawi na maganda ya michikicha.
8. Kujenga nyumba na kulima.
9. Kugharamia ndoa huchangia pakubwa kwa ndoa za mapema; ukiukaji wa haki za binadamu,wanawake kuchukuliwa kama wasiojiweza na pia kulazimisha wasichana kutopata elimu, kiangazi kinapotokea,wanaume huenda malishoni mbali na familia zao kwa kipindi kirefu, majukumu mengi kuachiwa mwanamke.
10. 

i. kujitambulisha-kujieleza/kujifahamisha

ii. kunadhifisha-kuwa safi

iii. uchumba-makubaliano baina ya mwanamke na mwanamme kabla ya kuoana

iv. kulipa mahari-malipo yanayotolewa na mvulana kwa msichana ili amwoe.

v. Sanda- kitambaa kinachofunikwa maiti.

vi. kukidhia mahitaji-kuweza kutosheleza mahitaji

## MAPISHI YETU

**Funzo 3**: Ufahamu – Mapishi yetu

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kusoma kifungu kilichomo akizingatia kanuni za usomaji bora.
- Kupanua msamiati wake na kuutumia ipasavyo.
- Kujibu maswali kwa usahihi.
- Kutambua jamii zinazomzunguka.
- Kujua mila, tamaduni na itikadi muhimu katika jamii yake.
- Kutathmini mila, tamaduni na itikadi za jamii mbalimbali.

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali ya dodoso kuhusiana na vyakula?
- Waelekeze wanafunzi kwenye maswali ya kifungu na kuwaagiza kuyasoma yote.
- Waelekeze kwenye kifungu na kuwaambia wakisome kimya.
- Baadaye chagua mmoja mmoja wasome kifungu kwa sauti.
- Waongoze kujadili masuala yanayotokana na kifungu hasa msamiati mgumu na tamathali za semi.
- Waelekeze kutunga sentensi wakitumia msamiati na tamathali hizo.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa ushauri unaofaa.

**Majibu**

1. Matunda; mboga na nafaka
2. Matawi; maganda na mizizi
3. Matunda hutupa vitamini ambayo inatukinga dhidi ya magonjwa.
4. *Tamayya; Basic; AsidaMiris Sharmout Abiyad; Kajaik; Asseeda* au *Asseeda Dukun.*
5. Uji ndio mlo muhimu Sudan Kusini na ndio kiamsha-kinywa na chakula cha kila wakati.
6. *Basico;* Huandaliwa na *kabila la Kuku a*mbao ni wenyeji wa

*Kajokeji.*

7. i. *Miris* - unaotengenezwa kutoka kwa mafuta ya kondoo na *okra* iliyokauka.
   ii. S*harmout Abiyad* - hutengenezwa kutoka kwa nyama iliyokaushwa.
   iii. *Kajaik* ambao unatengenezwa kutoka kwa samaki waliokaushwa.
8. Kushiriki mahali ambapo kuna mapishi ili ujifunze kupika na kuuliza maswali ya upishi
9. Vyakula vyenye mafuta mengi,sukari,keki na vyakula vyote vinavyoathiri mwili wako.
10. Mwanafunzi ataje aina ya chakula cha kienyeji akijuacho na aeleze jinsi ya kukiandaa.

## KUANDIKA

**Funzo** : Utungaji wa kiuamilifu - Resipe

**Malengo maalum**: Baada ya funzo, mwanafunzi aweze:

- Kueleza muundo wa insha ya resipe.
- Kuandika resipe.

**Vifaa**
Mifano mbalimbali ya resipe

**Utaratibu**

- Waulize wanafunzi maswali kuhusu umuhimu wa mupishi.
- Ukitumia mifano ya resipe, wafafanulie namna zinavyoandikwa.
- Waambie wakueleze sababu za kuandika resipe.
- Waongoze kupitia ufafanuzi uliomo huku ukiwapa mifano zaidi.

**Tathmini**

Waelekeze kufanya zoezi lililomo kisha ulisahihishe na kuwapa mashauri

zaidi.Hakikisha mwanafunzi ameandika:

1. Njia ya kuandaa chakula cha kienyeji akipendacho.

**Kazi ya ziada**

**Mwanafunzi aandike insha kuhusu:**

1. Kisa juu ya uzuri wa mila na utamaduni wa kwao.

2.Maisha ya kiamboni ni bora kuliko ya mjini.Jadili.